**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**06** **URAIA NA MAADILI**

**Muda: Saa 1:30** **SULUHISHO** **Mwaka: 2021**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu mbili; A na B zenye jumla ya maswali **sita (06)**
2. Jibu maswali **yote**


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org

***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***

SEHEMU A (Alama 26)

1. Jibu vipengele (i) – (v)

(i) Yapi kati ya yafuatayo ni makundi maalumu?
A. Wazee, watoto na walemavu
B. Watoto, matajiri na walemavu
C. Wafanyakazi, maalbino na wazee
D. Watoto, akinababa na walemavu
**Jibu: A. Wazee, watoto na walemavu**
Sababu: Makundi maalumu ni wale wanaohitaji huduma maalumu au ulinzi zaidi kutokana na umri au hali ya mwili, kama wazee, watoto na walemavu.

(ii) Ni tendo gani linalooonesha uwajibikaji wa watoto katika familia?
A. Kununua sare za shule
B. Kusaidia kazi ndogondogo za nyumbani
C. Kucheza mpira shuleni na nyumbani
D. Kujisomea muda wote
**Jibu: B. Kusaidia kazi ndogondogo za nyumbani**
Sababu: Kusaidia kazi ndogondogo za nyumbani ni uwajibikaji wa mtoto katika familia.

(iii) Mahitaji matatu ya msingi ambayo yanapaswa kutolewa na wazazi kwa watoto wao ni pamoja na:
A. Malazi, afya na ajira
B. Kitanda, chakula na ulinzi
C. Makazi, mkate na malazi
D. Chakula, mavazi na malazi
**Jibu: D. Chakula, mavazi na malazi**
Sababu: Chakula, mavazi na malazi ni mahitaji ya msingi kwa kila mtoto.

(iv) Gabo alaipokutana na Bibi kizee, alimsalimia na kumsaidia kubeba mzigo wake, tendo alilofanya Gabo ni kati ya matendo yanayoonesha nini?
A. Kumsaidia
B. Uadilifu
C. Wizi
D. Woga


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***

**Jibu: A. Kumsaidia**
Sababu: Kumsaidia bibi kizee ni tendo la huruma na msaada, si wizi au woga.

(v) Pamela alitoa taarifa kwa mama yake kuwa alikuwa amevunja sahani. Tendo la kutoa taarifa alilofanya Pamela linaonesha tabia gani?
A. Kujipenda
B. Kuwa na upendo
C. Kuwa mkweli
D. Kuwa na huruma
**Jibu: C. Kuwa mkweli**
Sababu: Kutangaza ukweli baada ya kufanya kosa ni tabia ya uaminifu.

2. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuoanisha alama za Taifa

(i) Alama inayowakilisha uhuru na nuru inayoangaza nchi yetu
**Jibu: C. Mwenge wa uhuru**
Sababu: Mwenge wa uhuru unawakilisha uhuru wa Tanzania na mwanga unaoangaza taifa.

(ii) Alama yenye rangi nne ambazo ni kijani, bluu, nyeusi na manjano
**Jibu: A. Bendera ya Taifa**
Sababu: Bendera ya Taifa ina rangi nne hizo zilizowakilisha ardhi, maji, watu na utajiri.

(iii) Alama inayoonesha picha ya mwanamke na mwanaume upande wa kushoto na kulia
**Jibu: E. Nembo ya Taifa**
Sababu: Nembo ya Taifa ina picha ya mwanamke na mwanaume, ikiwakilisha wananchi.

(iv) Alama inayooonesha uzalendo wa Taifa
**Jibu: F. Wimbo wa Taifa**
Sababu: Wimbo wa Taifa huamsha hisia za uzalendo na umoja wa taifa.

3. Jibu vipengele (i) – (iv)

(i) Njia mojawapo ya kuhifadhi mazingira yetu ni (kukata miti, kuchoma misitu, kupanda miti)
**Jibu: kupanda miti**


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***

Sababu: Kupanda miti kunasaidia kuhifadhi mazingira na kupunguza uharibifu wa ardhi.

(ii) Amani anatapika. Yawezekana anasumbuliwa na (maumivu ya mguu, ugonjwa wa malaria, ugonjwa wa ngozi)
**Jibu: ugonjwa wa malaria**
Sababu: Kutapika ni dalili ya ugonjwa kama malaria, si maumivu ya mguu au ugonjwa wa ngozi.

(iii) Kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla ya kula ni kitendo cha (uaminifu, kujijali, heshima)
**Jibu: kujijali**
Sababu: Kunawa mikono ni hatua ya kujilinda na kujitunza afya.

(iv) Ili familia iweze kujipatia mahitaji yake muhimu inatakiwa kufanya nini? (kukata miti, kufanya kazi kwa bidii, kuhifadhi fedha benki)
**Jibu: kufanya kazi kwa bidii**
Sababu: Kufanya kazi kwa bidii husaidia familia kupata mahitaji muhimu.

SEHEMU B (Alama 24)

4. Jibu vipengele (ii) – (v)

(ii) Wagogo
**Jibu:** Mkoa wa Dodoma
(iii) Mwanza
**Jibu:** Mkoa wa Mwanza
(iv) Tabora
**Jibu:** Mkoa wa Tabora
(v) Wahaya
**Jibu:** Mkoa wa Kagera

5. Chunguza picha ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

(a) Wanafunzi kwenye hii picha wanafanya nini?
**Jibu:** Wanafunzi wanashiriki katika shughuli za kujifunza Pamoja.

(b) Unafikiri watoto hawa wapo katika mazingira yapi?
**Jibu:** Wana katika mazingira ya shule, ya darasani yenye usafi na mpangilio mzuri.


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***

(c) Ni faida ipi unayoweza kuipata unaposhiriki katika tendo lilioneshwa katika picha?
**Jibu:** Kupata elimu, kukuza mwili kupitia michezo, na kujifunza kushirikiana na wenzako.

(d) Taja jina la samani iliyopo pichani ambayo hutumiwa kuhifadhia vitabu
**Jibu:** Dawati.